UTENDAJI

# Maabara ya mifugo yatakiwa ijiendeshe

Tuzo Mapunda,
tmapunda@mwananchi.co.tz

**Dar es Salaam.** Wakala ya Maabara ya Maifugo nchini (TVLA) imetakiwa kufanya kazi kibiashara ili ijiendeshe badala ya kutegemea ruzuku kutoka serikalini.

Wito huo umetolewa na katibu mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia sekta ya mifugo, Tixon Nzunda ziara yake kwenye sekta hiyo ikiwa ni mara ya kwanza tangu alipoteuliwa kushika wadhifa huo Juni 8, mwaka huu.

Kupitia taarifa iliyotolewa na wizara hiyo jana, Nzunda aliitaka taasisi hiyo kujikita katika kazi kibiashara na kuzifanya kwa uadilifu mkubwa, hasa kusimamia vyema mashamba ya mifugo yanayovamiwa kwa kuhakikisha yanapimwa ili kuondokana na adha ya kuvamiwa na wananchi.

Mbali na kuimarisha mashamba ya mifugo, Nzunda ameelekeza mifumo ya utendaji kazi ya kielekroniki katika ukusanyaji maduhuli iimarishwe katika vituo vyote vya Wakala hiyo.

Akielezea kuhusu changamoto ya uhaba wa watumishi wa wakala hiyo, Nzunda amemwelekeza mtendaji mkuu wa Wakala hiyo kufuatilia maombi ya kuajiri watumishi wapya katika Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma ili kukidhi mahitaji ya taasisi hiyo.

Vilevile Nzunda ameelekeza kulindwa na kutunzwa kwa mali za wakala hiyo ili ziweze kutumika kwa malengo yaliyokusudiwa.

Aliielekeza Wakala hiyo kufanya kazi kwa karibu na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini (GCU) cha Wizara ya Mifugo na Uvuvi ili kutangaza kazi nzuri zinazofanywa na wakala hiyo.

Katibu mkuu ameielekeza Wakala hiyo kukutana na wadau wanaotumia chanjo za mifugo kila mwaka ili kupata mrejesho kutoka wadau hao.

Alihitimisha maelekezo yake kwa kuitaka wakala ijikite katika kutafuta masoko ya chanjo hizo nje na ndani ya nchi.

### Kazi za Wakala

Awali, akisoma taarifa fupi ya Wakala, Mtendaji wake mkuu, Dk Stela Bitanyi alisema kazi wanayofanya ni uchunguzi na utambuzi wa magonjwa ya wanyama na wadudu wanaosambaza magojwa na uhakiki wa usalama na ubora wa vyakula vya mifugo.

Alisema wakala unatimiza majukumu yake kwa kupima, kutathimini na kuhakiki vitendanishi, mimea tiba pamoja na kemikali zinazotumika katika maabara za wanyama.

ZAIDI >

## TVLA pia inazalisha chanjo za mifugo

Kupitia Taasisi ya Chanjo nchini (TVI), Wakala ya maabara za Mifugo ( TVLA) inatengeneza na kuzalisha aina saba ya chanjo dhidi ya magonjwa ya mifugo pamoja vitendanishi.

Chanjo hizo ni Temevac (chanjo dhidi ya mdondo), kimeta, kimeta cha mbavu, Tecoblax (mchanganyiko wa kimeta na chambavu), kutupa mimba (Brucellosis), homa ya mapafu ya ng'ombe na homa ya mapafu ya mbuzi (CCPP).

# Daraja Tanzanite rasmi kesho bila malipo

Peter Elias, Mwananchi
pelias@mwananchi.co.tz

**Dar es Salaam.** Daraja jipya la Selander linalojulikana kama "daraja la Tanzanite" litaanza kutumika rasmi kesho baada ya kukamilika kwa asilimia 100 na hakutakuwa na malipo yoyote kwa watumiaji.

Akizungumza wakati akikagua daraja hilo jana, Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Profesa Makame Mbarawa alisema daraja hilo linalokatiza katika bahari ya Hindi litakuwa suluhisho la changamoto ya msongamano wa magari katika barabara ya Ali Hassan Mwinyi.

"Flow ya magari wakati wa alfajiri na jioni huwa si nzuri katika barabara ya Ali Hassan Mwinyi, daraja hili litawafanya watu wawahi maofisi asubuhi na kuwahi kurudi majumbani wakati wa jioni," alisema.

Waziri Mbarawa aliwataka wananchi kulitunza daraja hilo na kwamba Serikali itasimamia jambo hilo ili kama daraja limesanifiwa kuishi miaka 100, basi liweze kuishi hadi miaka 125.

Mtendaji Mkuu wa Tanroads, Rogatus Mativila alisema daraja hilo limekamilika kwa asilimia 100 kwa gharama ya Sh243 bilioni.

"Tunatarajia Februari mosi kulifungua daraja hili ili wananchi waanze kulitumia," alisema Mativila.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Aisha Amour aliwataka wananchi kulitunza kwa matumizi sahihi.

**1,030**

Urefu katika mita (sawa na kilometa moja na mita 30) wa daraja jipya la Tanzanite linaloanza kutumika kesho.

**KM5**

Urefu wa barabara iliyounganishwa na daraja jipya la Selender, linaloitwa Tanzanite ambalo linaanza kutumika kesho.




Scanned with CamScanner